

UKWELI


KUHUSU MIVUKE

Kunapatikana aina nyingi tofauti za sigara za kielektronik au 'mivuke' (vapes).

Kosa kubwa la kuelewa kuhusu mivuke ni kwamba hazina madhara ikilinganishwa na sigara.

Hii si kweli. Mivuke si salama. Kugundua mivuke kunaweza kuwa ngumu kwa sababu mara nyingi hufanana na vitu vya kawaida vya shule kama vile kalamu za kuangazia, viweka alama na viendeshi vya USB. Kujua maumbo na aina mbalimbali za mivuke ni hatua ya kwanza ya kusaidia kuwalinda vijana kutokana na hatari za mivuke.

MIVUKE YA KAWAIDA



Mivuke inayoweza kutupwa ndiyo ni mivuke ya kawaida zaidi kutumiwa na vijana. Inaweza kuwa kati ya 'mivuto' 300 hadi zaidi ya 4,000 ndani kila kifaa. Mara nyingi inatofautisha ya bei kuanzia \$15 hadi \$50, kutegemea idadi za 'mivuto' ndani ya kifaa. Mivuke hii mingi ina nikotini ndani, ingawa mara nyingi haina lebo ya kuonyesha ina nikotini ndani yake.



Mivuke inaweza pia kupatikana katika vifaa vya aina za ganda au vinavyoweza kujazwa tena, ambapo mtumiaji hujaza tena kifaa kwa majimaji ya kielektroniki au maganda mapya yaliyo na vimiminika vya kielektroniki. Vifaa hivi havionekani kuwa maarufu kwa vijana.



Je! Unajua wanavuta nini?
Pata ushahidi* na ukweli kwenye health.nsw.gov.au/vaping

* Taarifa zote zina msingi wenye ushahidi ambao unaweza kupatikana kwenye tovuti ile.

